

# TANGAZO

## MSIMAMIZI WA UCHAGUZI WA HALMASHAURI YA MJI WA MBULU ANAWATANGAZIA WANANCHI NAFASI ZA KAZI ZA MUDA KWA AJILI YA KUENDESHA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA MWAKA 2019.

TAREHE 13/09/2019

### 1. NAFASI YA MWANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA (NAFASI 210)

#### *Sifa za mwombaji*

- Awe Mtumishi wa Umma
- Awe mwaminifu na mwadilifu
- Asiwe mtendaji wa Kijiji, Mtaa au Kata
- Asiwe mshabiki wa chama chochote cha siasa
- Awe na uwezo wa kuwepo katika kituo cha uandikishaji kuanzia saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni

#### *Majukumu*

- Kuandikisha Wapiga Kura kwa muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe 08-14/10/2019
- Kufungua kituo cha uandikishaji wa Wapiga Kura kwa wakati kuanzia saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni.

#### *Jinsi ya Kuomba*

- Andika Barua kwa Msimamizi wa Uchaguzi
- Ainisha Kata na Kijiji au Mtaa uliopo na Check Namba yako
- Barua zote zipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kata husika
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **20/09/2019**

### 2. NAFASI YA MSIMAMIZI WA KITUO CHA UCHAGUZI (NAFASI 210)

- Awe Mtumishi wa Umma
- Ikiwezekana awe mkazi wa Kata atakayofanyia kazi
- Awe mwaminifu, mwadilifu, mvumilivu, mwenye hekima, busara, msikivu na anayejituma
- Asiwe mtendaji wa Kijiji, Mtaa au Kata
- Asiwe mshabiki wa chama chochote cha siasa
- Awe tayari kutoa msaada kwa wapiga Kura wote bila upendeleo wala ubaguzi wa aina yoyote
- Ainisha Kata na Kijiji au Mtaa uliopo na Check Namba yako
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **16/09/2019**

#### *Majukumu*

- Kupokea na kutunza vifaa vya Uchaguzi
- Kuandaa na kufungua kituo cha Kupigia Kura saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni
- Kuhakikisha kwamba Watendaji wa Kituo wanafahamu majukumu yao
- Kutoa ushauri na maelekezo kwa Wapiga Kura pale inapohitajika
- Kuhesabu Kura
- Kuhakikisha mawakala waliopo kituoni wanapewa fursa ya kujaza fomu zinazohisika

- Kushughulikia malalamiko yanayojitokeza Kituoni
- Kujaza fomu za matokeo na kuzibandika baada ya kusainiwa na Mawakala katika Kituo.
- Kumtangaza Mwenyekiti wa Kitongoji aliyeshinda kwenye kituo ambacho nafasi hiyo inagombewa
- Kuwasilisha taarifa ya Uchaguzi huo kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Mtaa/Kijiji baada ya ujazwaji wa fomu za matokeo ili Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi afanye majumuisho kupata mshindi wa jumla.

#### **Jinsi ya kuomba**

- Andika barua kwa Msimamizi wa Uchaguzi
- Ainisha sehemu ulipo (Kata), uzoefu katika shughuli za Uchaguzi na nakala ya Cheti cha Kidato cha nne (4)
- Barua zote zipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kata husika

### **3. NAFASI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO CHA UCHAGUZI (NAFASI 210)**

#### ***Sifa za mwombaji***

- Awe Mtumishi wa Umma
- Ikiwezekana awe mkazi wa wa Kata atakayofanyia kazi
- Awe mwaminifu, mwadilifu, mvumilivu, mwenye hekima, busara, msikivu na anayejituma
- Asiwe Mtendaji wa Kijiji, Mtaa au Kata
- Asiwe mshabiki wa chama chochote cha siasa
- Awe tayari kutoa msaada kwa Wapiga Kura wote bila upendeleo wala ubaguzi wa aina yoyote

#### ***Majukumu***

- Kumsaidia Msimamizi wa Kituo
- Kwa kushirikiana na Msimamizi wa Kituo kupokea na kutunza vifaa vya Uchaguzi
- Kuandaa na kufungua kituo saa mbili (2) asubuhi hadi saa kumi (10) jioni
- Kutoa ushauri na maelekezo kwa wapiga Kura pale inapohitajika
- Kumsaidia Msimamizi wa wa Kituo kuhesabu Kura
- Kushughulikia malalamiko yanayojitokeza Kituoni

#### ***Jinsi ya Kuomba***

- Andika barua kwa Msimamizi wa Uchaguzi
- Ainisha sehemu ulipo (Kata), uzoefu katika shughuli za Uchaguzi na Check Namba yako
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **16/09/2019**
- Barua zote zipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kata husika

Tangazo hili limetolewa na:

**HILARY G.MAKUNDI  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA MBULU MJINI**

**NB.Tangazo hili linafuta tangazo la tarehe 09/09/2019**